
- Ondoa maua yote yanayochipua katika mwaka wa kwanza ili kuwezesha mkorosho kukua.



- Kagua kila mkorosho mara moja kwa mwezi.
- Endelea kuondoa matawi hadi mkorosho ufikishe shina lenye urefu kati ya mita moja na mita moja na nusu. Mikorosho ikifikisha urefu huo iache itengeneze kivuli.
- Upogoleaji hukamilika ndani ya miezi sita ya kwanza tangu kupandikizwa kwa kutegemea utunzaji na mazingira ya sehemu husika.



**Mkorosho mchanga uliopogolewa vizuri wakati wa kukua unategemewa kutoa mazao mengi**

# UPOGOLEAJI MIKOROSHO MICHANGA ILIYOBEBESHWA



*Kimetayarishwa na:*


Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz


April 2019

## 1. UTANGULIZI

Kupogolea mche mchanga ni kitendo cha kukata mikorosho ya pembeni na kuuwezesha ukue kuelekea juu na kutengeneza umbo linalotakiwa. Kilele cha shina la mkorosho uliopandwa kwa mbegu kina uwezo wa kukua wima tokea kuota kwa mbegu hadi umri wa kukomaa.Lakini tawi la kileleni la mche uliobebeshwa halina uwezo huo hivyo matawi ya pembeni hutambaa sambamba na usawa wa ardhi. Mara nyingi kilele hudumaa.



## 2. FAIDA ZA UPOGOLEAJI

- Kuuwezesha mkorosho ukue wima
- Kutengeneza umbo la mwamvuli na hivyo kuepuka hasara zitakazojitokeza baadaye.

## 3. HASARA ZA KUTOKUPOGOLEA

- Mikorosho isipopogolewa katika hatua za awali za ukuaji huwa kikwazo baadaye kwa shughuli nyingi shambani mfano: kuokota korosho, palizi na udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu.
- Matawi yakishakomaa huwa vigumu kuyawekea nguzo na yakilazimishwa huvunjika.
- Kuchelewa kupogolea matawi mikorosho iliyobebeshwa baada ya miaka miwili hadi mitatu tangu kupandwa, humpunguzia mavuno mkulima anapopogolea kwa wakati huo.

## 4. JINSI YA KUPOGOLEA

- Kupogolea huanza mara tu baada ya miche iliyopandikizwa kutoa matawi.



- Pogolea kabla matawi hayajafikia unene wa kalamu ya risasi, ama wahi kukata vitawi vikiwa viteke kwa kutumia wembe au kisu chenye makali.

- Simika nguzo karibu na shina, funga mkorosho kwa kamba ili usiyumbishwe na upepo.

*Angalizo*

- Usiache matawi mpaka yakafikia kukomaa, utasababisha mti upoteze nguvu nyingi kukuza matawi ambayo hatimaye yatapogolewa.
- Unapokata tawi usikate jani lililopo chini yake, liache liendelee kutengeneza chakula cha mmea.

- Dhibiti mashambulizi ya mbu wa mikorosho kwa kutumia kiuatilifu kinachopendekezwa.